



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI



Simu; +255 (027) 2538006 (G/L)
+255 (027) 2538005 (D/L)
Nukushi: +255 (027) 2538136/361
Barua pepe: ded@mondulidc.go.tz
Tovuti: <http://www.mondulidc.go.tz>
Unapojibu tafadhali taja

Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P 1,
MONDULI.

Kumb. Na. HW/MON/C7/8/138

Tarehe: 22.02.2022

TANGAZO

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli anapenda kuwatangazia Ajira ya Muda mfupi kwa nafasi za wakusanya Taarifa kwenye zoezi la Anwani za Makazi katika Kata na Vijiji/Mitaa yote ya Wilaya ya Monduli.

A. SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe Raia wa Tanzania mwenye Umri kuanzia **Miaka 18 hadi 35**
- ii. Awe na Elimu kuanzia kidato cha Nne na Kuendelea
- iii. Awe anamiliki simu janja (inayotumia Android) na yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa siku nzima.
- iv. Awe na barua pepe (email address) inayotumika.
- v. Awe uwezo wa utambuzi wa maeneo ya mitaa/Kijiji husika
- vi. Awe ni Mkazi wa Mtaa/Kijiji husika

B. KAZI NA MAJUKUMU

1. Kugawa/kuandika Namba za Nyumba, Viwanja na Maeneo ya Huduma
2. Kukusanya taarifa za Nyumba, Viwanja na Maeneo ya huduma
3. Kukusanya taarifa za Wamiliki wa Nyumba, Viwanja na Maeneo ya huduma kwa kutumia Mfumo wa Anwani za Makazi.
4. Kutuma Taarifa kwenye Mfumo wa Anwani za Makazi kwenda kwenye Kompyuta Kuu.

C. MALIPO

Kazi hii itafanyika kwa muda wa siku 20 kwa malipo ya Shilingi laki mbili (200,000/=).

D. MAOMBI YAAMBATISHWE NA;

- i. Nakala ya cheti cha kidato cha Nne na Kuendelea
- ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa / Nakala ya Kitambulisho cha Nida au barua ya utambulisho kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa.
- iii. Picha (Passport size 2) za rangi.

E. JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na Anwani kamili ya mwombaji, namba ya simu, Barua pepe na zipitie kwa Watendaji wa Mitaa/Kijiji na Kata anapoishi na ziwasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli kwa Anwani ifuatayo; -

**MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA WILAYA,
S.L.P 1,
MONDULI.**

F. TAREHE YA MWISHO KUPOKEA MAOMBI

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 28/02/2022 Saa 9.30 Alasiri.


Rose Mhina

**Kny: MKURUGENZI MTENDAJI (W),
MONDULI.**

**Kny. Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya Monduli**

Halmashauri ya Wilaya, S.L.P 1, Monduli. Simu: +255 (027)-2538006, +255(027) 2538005. Nukushi
+255 (027) 2538136/361. Barua pepe: ded@mondulidc.go.tz. Tovuti: <http://www.mondulidc.go.tz>